

UTANGULIZI

MAPITIO MAFUPI

Yakobo, mtumwa wa Mungu, na wa Bwana Yesu Kristo, kwa makabila kumi na mawili waliotawanyika; salamu. 2 Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; 3 mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. 4 Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno. (Yakobo 1:1-4)

Kanuni = "Usiulize kwa nini, uliza nini."

Maswali matatu kuhusu "nini" yanayoulizwa na watu wanaosalia imara:

1. Je, naweza kudhibiti nini maisha yangu yanaposambaratika?
2. Je, napaswa kufanya nini ili niweze kuipita siku ya leo vizuri?
3. Je, nina tumaini gani kwa ajili ya kesho?

Jibu = Ukuu wa Mungu + wema wake = Atachukua hali zangu mbaya zaidi na kuzitumia kuniletea hali bora zaidi ikiwa nitamtumainia na nisijiondoe kutoka kwenye mchakao wake wa kunikomaza kiroho..

1. **Tatizo – Wakati mwingine "tunakwama" katika maumivu yetu.**
2. **Suluhu – Mungu anaahidi msaada kwa wale ambao "wamekwama."**

Lakini mmoja wenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. 6 Ila na aombe kwa imani, pasipo mashaka yoyote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari linalochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. 7 Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. 8 Mtu wa nia mbili husitasita katika njia zake zote. (Yakobo 1:5-8)

- Kile anachotoa Mungu = HEKIMA Isiyo ya Kawaida
- Wajibu wetu = KUOMBA
- Mtazamo wa Mungu tunapomwomba = YUKO WAZI NA NI MKARIMU

3. **Sharti moja – Tunapokea hekima ya Mungu tu "tunapomba kwa imani pasipo kuwa na shaka."**

- Kuomba "kwa imani" kunamaanisha...
- "Pasipo kuwa na shaka" inamaanisha...

HITIMISHO – MAMBO MANNE AMBAYO LAZIMA UFANYE ILI UJIKWAMUE

1. Kubali kuwamba umekwama..
2. Kubali kwamba huwezi kufanya lolote peke yako.
3. Mwombe Mungu hekima isiyo ya kawaida.
4. Kuwa tayari kufanya lolote ambalo hekima ya Mungu itakuhitaji ufanye.

MASWALI YA MAJADILIANO

1. Kulingana na Maandiko, "hekima" ni nini? Je, hilo linatofautianaje na mawazo yetu ya kawaida na matumizi yetu ya neno hili?
2. Je, ni mtazamo gani unaojitokeza katika kifungu hiki kuhusiana na huruma ya Mungu na kuelewa kwake "kukwama" kwetu katika dhiki?
3. Jadili sharti moja linalohitajika ili kupokea zawadi hii isiyo ya kawaida ya hekima ili kukua kupitia maumivu katika majaribu yetu. (Tazama Yohana 7:17, Warumi 12:1)
4. Utahitaji kuchukua hatua gani ili kupokea hekima ambayo Mungu anaahidi kukupa katika hali yako ya sasa?